MWENYEKITI wa Libati Heroes Club Bw. Abeid K. Salim anatoa mkono wa Idd-el-Hajj kwa jamaa yake na Waislamu wote wa Mombasa kutoka Jedda Saudi Arabia akiwa safarini Kuhiji Makka.

Mkono wa Idd kwa Waislamu wote

Hii ni siku kuu ya kujifunza mausiyo ya kujitolea ili nyoyo za wanadamu zipate kunawirika na maendeleo ya nchi yazidi kupata msingi imara wa maendeleo.

Hii ni siku kuu ya kukumbushana mafunzo tulioletea na mitume yetu tokea Sayyidna Ibrahim, Sayyidna Ismail hadi Mtume SAW tunapokumbushana mema ndipo tutakapo ingiwa na moyo wa kufanyiana mema na kuzidihiana mapenzi nyoyoni mwetu.

Katika Risala hii ningependa nikokoteze jambo moja kwa vijana vyetu Waislamu. Jambo la wenyewe ni kuwausia wajitolee maisha yao kwa kutumikia umma wao kwa njia ya kuleta maendeleo, ufanisi. Kila kijana wetu akitia nia ya kwamba maisha yake yatakuwa ni kiungo cha mapenzi, umoja na amani basi atakuwa ameshiriki vyema katika kueneza Philosophia ya Nyayo kama tulivyousiwa na Mtukufu Rais Moi.

Nguvu zetu, matumaini yetu, imani yetu na maendeleo yetu yote yamo katika mikono ya vijana vyetu waliotiwa imani, kupewa adamu ya mafunzo ya dini kwa njia ya ujenzi.

Yaarabi nchi yetu chini ya uwongozi wa Busara na Hekima ya Mtukufu Rais Daniel Arap Moi nchi yetu iwe ni yenye nuru ya maendeleo na ibaki iwe ni mfano wenye kuandamwa na nchi nyingine za Afrika. Mungu aitukuze nchi na viongozi wa nchi yetu.

Mohammed Salim Shirazy,
Tamimu wa Thalatha Twaifa Msa

Namna ya Kuhiji nguzo na ukamilifu wake

Na Sheikh Nassor Khamis

MWENYE kunuia Hija lazima au yampasa alete Talbiya baada ya kuvaa ihram zake. Talbiya yenyewe ni hii: *Labaika allahumma labaika, Labaika laa sharikalaka labaika; innalhamda waneemaka lakawalmulka laasharikalaka.*

Atayasema maneno haya mume au mke mpaka asubuhi ile ya kutupa vijiwe huko Mina. Hivi ndivyo ilivyothubutu kutoka kwa Mtume SAW. Na ni vizuri kwa yule aliyetoka safari ya mbali kama sisi tunaotoka Kenya kufanya Tamatui nako ni kukusanya Hija na Umra akiwa mtu huyo hakuchelewa na akafika kabla ya tarehe nane mfungo tatu. Yaani anuiye Umra kwanza, akifika Makka akatufu Al Kaaba na afanye Saayi kati ya Safaa na Marwa, kisha anyoe nyele au apunguze, hapo Umra huwa imekwisha na avae nguo zake za kawaida. Ikifika tarehe nane mfungo tatu watu wote huanza msafara wa Hija kutoka Makaa.

Watu siku hii hulala Mina, wakasali Adhuhuri, Alasiri, Magharibi, Isha na Alfajiri kwa kukusuru. Kisha asubuhi watu wanafunga msafara kwenda Arafa. Huko watu watasali Adhuhuri na Alasiri wakati mmoja kwa kukusuru kisha watu wangie katika uwanja wa Arafa kwa ajili ya kumuomba Mwenyezi Mungu mpaka jua litakapotua Magharibi. Kisha watu hufunga msafara hadi Muzdalifa huko watu watasali Magharibi na Isha. Ni kinyume kusali Magharibi njiani. Watu ni lazima walale hapo Muzdalifa hadi wasali Alfajiri. Baada ya kumuomba Mungu watu hapo huondoka kwenda Mina. Wakifika Mina huanza Ibada ya hapo kwa kurusha vijiwe huko Jamra vijiwe saba, halafu wachinje, halafu wanyoe au wapunguze nywele. Umalizapo hivyo, mambo mengi huwa ni halali kuyafanya isipokuwa kuonana na mkeo (kimwili). Na Mtume SAW siku hiyo hiyo alishuku kwenda Makka kutufu Tawaful Ifadha, ambayo ni nguzo ya Hija.

Halafu watu ni lazima wakae hapo Mina siku tatu, ukitoa ile siku ya Idd ile haihisabiwi. Yaani utakaa tarehe kumi na moja, kumi na mbili na kumi na tatu, siku zote hizo ukirusha vijiwe ishirini na moja. Bali yule aliye na safari ya haraka aruhusiwa kuondoka siku ya tarehe kumi na mbili baada ya kusali adhuhuri na kurusha viiiwe. Ikiwa mtu hakuyakamilisha hayo ajue kwamba hija yake haikukamilika na kwa hivyo ni lazima akalipe mwakani.

Mambo yanayoharimishwa kwa mwenye Kuhiji.

Ni haramu kwa yule mwenye kuwa katika Ibada ya Hija kufanya haya yafuatayo:

•Kuundama, yaani kuingiliana na mkewe, au kufanya jambo lolote ambalo laweza kuwa ni sababu ya kufanya kitendo hicho, kama kubusu, kumshika kwa matamanio au kutongoza.

• Kutoka katika twaa ya Mwenyezi Mungu na kufanya vile unavyotaka wewe. Inagawaje jambo hili wakati wowote halifai, lakini katika hija ni zaidi, kwani utakuwa umekwenda kutembea tu hukwenda kuhiji.

• Kuteta na watu na kujadiliana mambo yasiyokuwa na msingi wa kidini.

• Kuvaa nguo iliyoshonwa. Yaani ni haramu kwa yule anayehiji kuvaa shati ama kanzu, kilemba, suruali, pajama, kofia viatu vya buti au nguo yoyote iliyoshonwa inayozunguka mwili wa Binadamu. Na hayo ni kwa mwanamume peke yake. Ama mwanamke yaruhusiwa kwake asitiri mwili wake wote kwa kila chenye kusitiri, kiwe kimeshonwa au hakikushonwa.

• Vile vile ni haramu kwa mwenye kuhiji kuondosha nywele zake kwa kuzinyoa au kwa kuzifumua, tena kila jinsi ya nywele za kichwani na nyenginezo, na ikiwa ataondosha nywele zake basi itamlazim mtu huyo fidya, yaani achinje mnyama au afunge siku tatu au amlishe masikini. Vile vile kukata kucha pia haifai kama kunyoa. Vile vile kufunika kichwa kwa kofia ama kwa utaji. Haya tu kwa ufupi ndiyo yatayomlazimu mwenye kuhiji, ayatende ili Hija yake iwe kamilifu. Hatahivyo nataka kuongeza mambo yanayohusiana na Tawafu.

Kuna nanma tatu kuitufu Nyumba tukufu ya Alkaaba. Ya kwanza ni Tawafu ya maamkuzi; nayo ni ile anayoitekeleza mtu anapofika Makka na hii ni kama Tahiyatul Masjid. Ya pili ni Tawaful Ifadha. Na hii ni nguzo ya Hija. Kwa hivyo iwapo Mhujaji hakutufu Tawafu hii basi ajue inayotekelezwa baada ya kutoka Arafa na Muzdalifa na baada ya kurusha vijiwe na kuchinja na kunyoa nywele au kupunguza. Ya tatu ni tawafu ya kuaga. Hii hufanyika pale mtu anapotaka kuondoka Makka baada ya kumalizika wajibati za Hija. Ni mamoja iwapo mhijaji yuarudi nyumbani ama anaelekea madina ni lazima atufu Tawafu ya kuaga ilivyokuwa hatarejea hapo.

Masahrti ya Tawafu

Ili tawafu yako katika nyumba hiyo tukufu ikamilike, ni lazima ukamilishe masharti haya: Kwanza utahirike na haddathi na najisi. Yaani tawafu haisihi iwapo anayetufu hana udhu au hakutahirika na janaba, vile vile iwapo nguo ina najisi au mwili wake umegandama najisi. Hii ina mana kwamba hata ikiwa mwanamke ana ile ada yake ya kila mwezi, hawezi kufanya tawafu mpaka ada yake isite, ndipo atufu. Pili ni lazima asitiri tupu yake kama vile anavyojisitiri wakati wa kusali. Tatu ni lazima akamilishe mizunguko saba, akifanya nusu basi tawafu yake haikusihi kabisa. Nne ni lazima tawafu yake iwe ndani ya msikiti, asione watu wamejazana, kama siku hizi akaona ni heri atufu nje ya msikiti, hayo hayafai. Jambo la tano ni kuwa aanzie tawafu yake kwenye Hajaril Aswad, na ni lazima hiyo Alkaaba iweko kushotoni kwake (kinyume cha mkono wa saa unavyozunguka) hadi amalize mizinguko yake.

ATARAJIAMALIPO

Akiyatimiza haya na yale mengine tuliyoyataja huko nyuma basi mtu huyo atakuwa amekamilisha Hija yake atarajia malipo yake kwa Mwenyezi Mungu Mola wetu. Nawatakia Waislamu wenzangu Hija njema, pia nawakumbusha Waislamu wa nchi yetu ya Kenya, wafikapo katika sehemu tukufu hizo za Makka waiombee Nchi yetu amani, umoja na mapenzi — mwito wa Rais wetu.

Viroja vya kijana Omari na Bonzo "Jimmy Boy" vitakuwapo katika ukumbi wa makadara wakati wa shamra shamra za Idd-El-Hajj.
PICHA: ABEID KARAMA.

UTEUZI WA HARAMBEE STARS SI WAKURIDHISHA

MENGI HUSEMWA WAKATI timu ya taifa inapochaguliwa kwa ajili ya matayarisho ya wachezaji watakaowakilisha Kenya katika michuano ya Challenge Cup ambayo hushindaniwa katiya nchi kadha za Afrika Mashariki na Kati. Malamiko mengi yameanza kusikika kutokana na uteuzi uliofanywa wa wachezaji watakaowakilisha Harambee Stars katika mashindano hayo.

Sidhani kama kuna mwaka wowote uliopita ama utakaokuja kwa mashabiki na viongozi wanaohusiana na kandanda kutoa lawama kwa wachezaji watakaochaguliwa kuwakilisha taifa kwa matayarisho ya mashindano ya Challenge Cup na mengineo. Lakini hata ikiwaje, hakuna kiongozi yoyote wa chama cha soka nchini ama mwingine anayeweza kuridhisha kila shabiki anayependa soka katika uteuzi wake.

Kijana wetu wa Pwani, John Arieno anayecheza nafasi ya Sentahafu katika timu ya Kenatco ni mchezaji wa pekee aliyeonekana kustahili kuwakilisha taifa ambaye ametajwa kujiunga na wenzake kwa matayarisho ya kujiandaa kwa michuano ya kombe la Challenge yatakayofanyika mjini Kampala, Uganda mwaka huu. Swali ni je, katika timu zote zinazoshiriki katika ligi za ngazi tofauti Pwani, ni mchezaji mmoja pekee aliyestahili kuwakilisha taifa hili? Swali hilo ni rahisi kujibika na jibu lake ni la hasha! Arieno ni kijana mshupavu anayestahili kucheza Harambee Stars na kuna wengine ambao hawakutajwa walio na ujuzi wa hali ya juu wa kuliwakilisha taifa lakini pengine hawakupata nafasi ya kujitambulisha kwa kuwa hawachezei timu kubwa.

Hapo zamani timu yetu iliyokuwa na miamba kadha kutoka Pwani akina Ali Kajo, Jabir Ali Riziki, Ali Sungura, Badi Ali, Ahmed Breik, Nassir Omar, Kadir Farrah, Mahmood Mohammed na Amrani Shiba ilikuwa rahisi kufanya uteuzi kwa sababu wengi wao walipata nafasi nyingi za kucheza mechi katika kila pembe ya Jamhuri katika mashindano ya ligi ya taifa pamoja na kuwakilisha mikoa yao katika mapambano ya Kenyatta Cup ambayo hapo awali yalikuwa yakijulikana kama Remington Cup.

Ni lazima Shirikisho la Soka la KFF lifanye taratibu za kufufua mashindano ya Kenyatta Cup ili vijana chipukizi walio na maarifa ya kulisakata soka la kisasa na wanaochezea timu zisoshiriki kwenye Supaligi wapate fursa ya kuwakilisha mikoa yao ili wateuzi wawaone na wakistahili kuchezea Harambee Stars wapatiwe nafasi zao. Ikiwa KFF itazingatia vile mipango ya miaka ya nyuma ilivyokuwa ikifanyika wakati timu za Supaligi kuruhusiwa kuandikisha wachezaji kutoka vilabu mbali mbali kuvipa nguvu, basi soka litarudia enzi za akina Jeo Kadènge na kutatokeza miamba ambao watapeperusha bendera ya Kenya katika mashindano ya kimataifa na kutuletea vikombe ambavyo hatujaviyakuwa kama kombe la nchi za Kiafrika na kupata nafasi ya kushiriki katika michuano ya fainali ya kombe la Dunia.

Namaliza kwa kuifahamisha KFF kwamba hakuna lisilowezekana, bora viongozi wake watimize wajibu wao wa kuongoza soka bila ya mapendeleo na nina uhakika vijana wengi kama alivyojitokeza Arieno wataonekana na kupata fursa ya kuchezea Harambee Stars.

— Absulrahman Sheriff

JISHINDIE

MIAVULI AU T-SHIRT MARIDADI KATIKA SHINDANO JIPYA LA KUJAZA MANENO

SWAHILI CROSSWORD NO 148



KWENDA KULIA:

1. Aina ya mnyama wa Australia
5. Chombo cha seremala
6. Mnyama wa kufugwa
8. Nchi huru Afrika
11. Funga ndoa
12. Fanya ili afuate mfano
14. Kiungo cha maneno
16. Mwangaza
17. Aina ya mtego wa samaki
18. Tamko la kukana

KWENDA CHINI:

1. Kata kwa msumeno
2. Tandiko
3. Kuwa juu ya maji
4. Shika, chukua
7. Namna ya madudu mfano wa konokono
9. Aibu, fedheha
10. Wewe
13. Mahali panapowekwa wanyama wakufungwa
14. Sehemu ya mwili
15. Stesheni kati ya Mombasa na Nairobi.

Washindi wa Fumbo la Kujaza Maneno No. 145

1. Mr. M. K. Kumenzwa, Sanduku la Posta 80149 Msa.
2. Abbas Mohamed Sanduku La Posta 85965 Mombasa.
3. Naazatun Ahmed Sanduku La Posta 81193 Mombasa.

Washindi waombwa wafike afisini mwa *COASTWEEK.*

MAJIBU YA SHINDANO LA FUMBO LA KUJAZA MANENO NO. 147 —

KWENDA KULIA:
1. KALANI, 5. WAO, 6. KINGA, 7. OTAMIA, 9. AU, 10. DAU, 12. NDIZI, 14. HUA, 15. WA, 16. ONGEZA.

KWENDA CHINI:
1. KIKULACHO, 2. LENGO, 3. NGAMANI, 4. KOJA, 5. WARIDI, 8. AA, 11. UTA, 12. NAO, 13. ZEE, 15. WA.

JINA ....

SANDUKU LA POSTA ....

....

Shindano la Fumbo la Kujaza Maneno:-

Uamuzi wa majaji utakuwa wa mwisho. Hakuna malalamiko yoyote yatakayokubaliwa. Washindi watatu kila baada yawiki mbili watapata miavuli au T-shirt maridadi. Shindano hili limeshaminiwa na *COASTWEEK* Limited Mombasa.
Jawabu za Fumbo hili lipekelwe kwa Muhariri *COASTWEEK* Sanduku La Posta 87270, Mombasa Kenya.
Siku ya Jumatano tarehe October 6, 1982 saa nne asubuhi shindano hili litakuwa mwisho.